# JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

# FAHARI YA SAME MAENDELEO DAIMA

## KIONGOZI MBIO ZA MWENGE AIPONGEZA SAME KWA UBORA WA MIRADI



*Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro,Mhe.Nurdin Babu akikabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Mkuu wa Wilaya ya Same Mshikizi,Mhe.Amir Mkalipa baada ya kuupokea kutoka Mkoa wa Tanga*

Kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa 2023 Ndg. Abdallah Shaib Kaim ameeleza kuridhishwa na Ubora wa Miradi saba ya Maendeleo aliyoitembelea katika Wilaya ya Same wakati Mwenge wa Uhuru ulipokimbizwa Wilayani humo.

Mwenge wa Uhuru uliwasili na kukimbizwa katika Wilaya ya Same Juni 20 mwaka huu, ambapo Mwenge huo ulifikia Miradi saba ikiwemo Miradi ya Afya,Maji,Elimu,Mazingira, Barabara na Ujasiriamali yenye thamani ya shilingi Bil.3.68.

Akizungumza baada ya kukagua Miradi hiyo, Kiongozi wa Mbio za Mwenge Ndg.Abdallah alisema ameridhishwa sana na Ubora wa Miradi na mpangilio mzuri wa Nyaraka za Miradi yote iliyofikiwa na Mbio za Mwenge.

“Tumefanya Ukaguzi wa kina wa Miradi na Nyaraka,tumejiridhisha na Ubora na thamani ya fedha,niwapongeze sana Mkuu wa Wilaya,Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi kwa usimamizi makini wa Miradi” alisema Ndg.Abdallah.

Awali akipokea Mwenge wa Uhuru Mkoani Kilimanjaro ukitokea Mkoa wa Tanga, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe.Nurdin Babu alisema, ukiwa Mkoani Kilimanjaro Mwenge wa Uhuru utafikia Miradi 45 yenye thamani ya shilingi Bil.30.3 na utaanza kukimbizwa katika Wilaya ya Same.

Baada ya Mkuu wa Mkoa kupokea Mwenge wa Uhuru, aliukabidhi Mwenge huo kwa Mkuu wa Wilaya ya Same Mshikizi, Mhe.Amir Mkalipa kwa ajili ya kuanza kuukimbiza katika Wilaya ya Same.

“Katika Wilaya ya Same tutakimbiza Mwenge wa Uhuru kwenye umbali wa Kilomita 102 na utafikia Miradi ya Maendeleo saba yenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 3.86” alisema Mhe.Amir.

Ukiwa Wilayani Same, Mwenge wa Uhuru uliweka jiwe la Msingi katika Ujenzi wa kiwango cha zege katika kona korofi za barabara ya Hedaru-Vunta –Myamba(mita 810)wenye thamani ya shilingi milioni 655.5.

Mwenge pia ulizindua madarasa mawili katika shule ya Sekondari Chauka yenye thamani ya shilingi mil.42.6, ambapo mil. 40 ni fedha za tozo, na mil 2.6 ni michango ya nguvu za wananchi.Katika shule ya Chauka Mwenge Ulizindua pia Klabu ya Wapinga Rushwa.

Ukiwa Wilayani Same, Mwenge wa Uhuru uliweka pia jiwe la Msingi katika Ujenzi wa Zahanati ya Saweni ambayo ujenzi wake umegharimu shilingi milioni 95,ambapo milioni 75 ni mapato ya ndani ya Halmashauri na mil 25 ni nguvu za wananchi. Mwenge pia ulitembelea Ujenzi wa Hospitali Mpya ya Wilaya ya Same ambayo katika awamu ya kwanza ujenzi wake umegharimu shilingi bilioni 2.

Miradi mingine iliyofikiwa na Mwenge Wilayani Same ni Mradi wa Maji Mwembe wenye thamani ya shilingi milioni 662.1, ambao ulizinduliwa pia Mwenge ulizindua Kitalu cha Miti TFS chenye thamani ya shilingi Mil.112.



*Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023, Ndg. Abdallah Shaib Kaim, akifungua bomba kuzindua kizimba cha maji Kirinjiko Sokoni, kinachohudumiwa na Mradi wa Maji Mwembe uliogharimu shilingi Milioni 662.1.*

# ACHENI KUVAMIA MAENEO YA SERIKALI-DC AONYA



*Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni, akizungumza na Wananchi wilayani humo.*

Mkuu wa Wilaya ya Same, Mhe.Kasilda Mgeni, amewaonya wananchi kuacha tabia ya kuvamia maeneo ya Serikali na kujimilikisha au kufanya shughuli zozote za Maendeleo.

Ametoa onyo hilo jana, wakati akizungumza na wananchi wa Kata za Vunta na Myamba ambapo amesema, katika maeneo hayo kumekuwa na tabia ya baadhi ya watu kuvamia na kulima ama kujenga katika maeneo ya Serikali.

“Afisa Tarafa hakikisha unakagua maeneo ya Serikali na iwapo utabaini Kuna uvamizi wowote hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahusika,hatuwezi kuvumilia kuona maeneo ya Serikali yanachukuliwa hovyohovyo"alielekeza Mhe. Kasilda.

Aidha, Mkuu huyo wa Wilaya amewataka wananchi kuungana na kufanya kazi kwa bidii, ili kuleta maendeleo katika Wilaya hiyo na nchi kwa ujumla.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Vunta, Mongera Kanyika, amemshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kuendelea kutatua kero mbalimbali zilizopo katika Kata hiyo.


## SAME YAPOKEA ZAIDI YA BIL 12 KUTEKELEZA MIRADI YA MAENDELEO 2022/2023



*Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Bi.Anastazia Tutuba, akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani*

Halmashauri ya Wilaya ya Same imepokea Shilingi Bilioni 12.9, kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Akizungumzia fedha hizo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bi.Anastazia Tutuba amesema, kati ya fedha hizo Shilingi Bil. 4.57, zimetoka Serikali Kuu na zilielekezwa katika Miradi mbalimbali, ukiwemo Mradi mkubwa wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya unaogharimu Bil 2 kwa awamu ya kwanza na ya pili ya Ujenzi huo.




Aliitaja Miradi mingine iliyotekelezwa kwa fedha hizo kuwa ni pamoja na Ujenzi wa bweni katika shule za Sekondari Same, ambao umegharimu shilingi mil.130 na Ukarabati wa mabweni mawili shuleni hapo ambao umegharimu shilingi.mil 150

.

Shughuli nyingine zilizofanyika ni umaliziaji wa mabweni mawili katika shule ya Sekondari Kimala mil 130 na umaliziaji wa Bweni shule ya sekondari Makanya ambao umegharimu shilingi mil.40.

“Fedha hizi toka Serikali Kuu pia zimetuwezesha kununua vifaa tiba, vyenye thamani ya shilingi mil 730 kwenye vituo vya Afya vitano na Zahanati tano pia zilitumika kumalizia ujenzi wa zahanati 4 ambapo kila moja ilitumia milioni 50” alisema Tutuba.

Mkurugenzi huyo anasema kuwa, fedha hizo pia zilitumika kujenga bwalo la chakula katika shule ya sekondari Kibacha, lenye thamani ya shilingi mil.100 na nyumba nne za walimu zilizogharimu mil.200 kwenye shule nne za Msingi.

Miradi mingine iliyotekelezwa na fedha hizo ni Ujenzi wa Madarasa saba katika shule ya Msingi Same, (Mil.160)na Madarasa matatu shule ya Sekondari Same (Mil.75) na Matundu 16 ya vyoo Kimala Sekondari na matundu 05 ya vyoo Same sekondari.
Amesema kuwa Halmashauri hiyo ilipokea pia shilingi Bil.1.36 kutoka Mradi wa SEQUIP, ambazo zilitumika kujenga nyumba mbili za Walimu (2 in 1) katika shule za Sekondari

Kalemawe na Mighareni ambazo kila moja iligharimu shilingi Mil.98 na shule mbili mpya za Sekondari za Kisima na Misufini, ambapo kila moja imegharimu Milioni 584.28.

Fedha nyingine zilizopokelewa kwa mwaka wa fedha 2022/23 ni pamoja na Fedha za Mradi wa BOOST, Tsh.Bil 1.86 kwa shule za Msingi ambazo zimejenga shule mpya mbili na madarasa 40, fedha za EP4R Mil.580,fedha za Tozo Mil 640, ambazo zimejenga madarasa 32 ya shule za sekondari,fedha za Mfuko wa Jimbo Mil. 129.9 na fedha za Ufadhili toka Barrick Goldmine, Mil 271.8 zinazojenga matundu ya vyoo.

"Kwa upande wa Mfuko wa TASAF fedha zilizopokelewa kwaajili ya Walengwa wa Kaya Maskini ni Shilingi Bil. 2.37, ambapo kwa upande wa mapato yetu ya ndani tulitenga shilingi Milioni 744, ambazo zimetumika katika Miradi mbalimbali ikiwemo uwezeshaji kiuchumi wa wanawake ,Vijana na watu wenye Ulemavu" alisema Tutuba.

## SAME YAPATA WATUMISHI WAPYA 196, DED AMSHUKURU RAIS DKT SAMIA



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Bi. Anastazia Tutuba.*

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Bi.Anastazia Tutuba amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia Wilaya hiyo watumishi wapya 196 kwa kipindi cha mwaka mmoja.

"Kwa kipekee kabisa, nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutupatia watumishi

wapya kwani, ongezeko hili linasaidia kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi" alisema Tutuba.

Mkurugenzi huyo alizitaja sekta zilizopata watumishi kuwa ni sekta ya Elimu Awali na Msingi, ambayo imepata watumishi 71 na Elimu Sekondari imepata watumishi 93 na wote wamesharipoti katika vituo vyao vya kazi.

Alisema sekta nyingine ambayo imepata nyongeza ya watumishi ni sekta ya Afya, ambayo imepokea watumishi 30, huku Halmashauri hiyo ikipokea Wahandisi wawili ambao wote wamepokelewa kuanzia Julai 2022 hadi June 2023.

Akizungumzia uhitaji wa watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Same, Mkuu wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Bi.Nice Ngasala, amesema kuwa Wilaya bado ina mahitaji ya nyongeza ya watumishi katika Sekta mbalimbali lakini zaidi sekta ya Elimu na Afya.

"Tunashukuru serikali kutukumbuka na kutuongezea watumishi, lakini bado tuna uhitaji wa watumishi kwenye idara mbalimbali husussan Elimu na Afya hivyo, tunaomba watakapoajiriwa wengine Serikali iendelee kutukumbuka" alisema Ngasala.

# TAMISEMI YAMWAGA VIFAA VYA ZAIDI YA MIL.20 KWA WAJASIRIAMALI SAME




*Mkuu wa Wilaya ya Same,Mhe.Kasilda Mgeni (wa pili kulia) akikabidhi seti ya Cherehani kwa kikundi cha Wanawake cha Kitamaka cha Kata ya Kalemawe,anayepokea kushoto ni kiongozi wa Kikundi hicho Bi.Amina Gadi, akiwa na wenzie,kikundi hicho kilipatiwa seti mbili za vyerehani.*

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Bi.Anastazia Tutuba, amesema halmashauri hiyo imepokea pikipiki mbili,vyerehani 10 na mashine za kuchomea 6 kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, ili kuwezesha uendelezaji wa viwanda vidogo na vya kati Wilayani humo.

Amesema, vifaa hivyo vya uwezeshaji wajasiriamali vimetolewa kwa Halmashauri 38 kati ya Halmashauri 184 zilizokaguliwa namna zinavyowezesha wajasiriamali kuanzisha viwanda vidogo na Same kuonekana imekidhi vigezo.

"Vipo baadhi ya vigezo vilivyoangaliwa ikiwemo, Halmashauri kutoa mikopo ya wanawake,vijana na watu wenye ulemavu kwa robo zote,uwezeshaji wa kuanzishwa viwanda vidogo,idadi ya vikundi vilivyowezeshwa na Maendeleo yake" amesema Tutuba.

Akikabidhi Vifaa hivyo kwa Wajasiriamali,Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni aliwataka wajasiriamali waliopewa vifaa kuvitunza vifaa hivyo na kuvitumia kwa malengo tarajiwa.

“Mheshimiwa Rais ameendelea kuwakumbuka wajasiriamali wa Same, hivyo naomba msimwangushe Rais katika matumizi ya vifaa hivi,vifaa hivi vikatumike kwa manufaa ya kikundi kizima na sio kunufaisha mtu mmoja mmoja kwenye kikundi”alionya Mkuu wa Wilaya.

Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Same, Bw. Benedict Missani, amesema kwa kipindi cha robo tatu za mwaka unaoishia Juni 2023, Wilaya ilifanikiwa kutoa mikopo ya shilingi milioni 310.5 kwa vikundi 75 vya vijana,wanawake na watu wenye ulemavu.

Amesema vikundi vya wanawake vilivyonufaika na mikopo hiyo ni 42, ambavyo vilipatiwa milioni 162,vikundi vya vijana ni 18, ambavyo vilikopeshwa milioni 101 na vikundi vya watu wenye ulemavu ni 15, ambavyo vilikopeshwa shilingi milioni 47.5.

"Vikundi hivi vyote tulivikagua na kujiridhisha kwamba vinastahili kukopeshwa na ndipo tulipovikopesha na vikundi hivi vinaendelea kufanya vizuri sokoni na hata kwenye marejesho.Lengo la Serikali ni kushawishi uanzishwaji wa Viwanda vidogo ”amesema Bw.Missani.

Vikundi vilivyonufaika na msaada huo ni Karawa Alluminium Vioo na Alluminium Vioo ambavyo kila kimoja kimepatiwa seti 3 za mashine za Alluminium.

Mgawo wa vyereheni umevinufaisha vikundi vya  Wanawake vya Kitamaka,Shengena, Sayuni,Upendo na Taarifa na Maarifa ambapo kila kimoja kimepata seti mbili za vyerehani na pikipiki mbili zimetolewa kwa maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata za Mpinji na Lugulu.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa seti tatu za mashine ya Alluminium,Mwenyekiti wa Kikundi Cha Alluminium Vioo, Bw.Nathan Mrema aliishukuru Serikali kwa kuwapatia vifaa hivyo, kwani wameongezewa mtaji wa kupanua zaidi biashara yao.

“Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa msaada huu kwani kikundi chetu kwa sasa kinapokea vijana wengi zaidi wanaokuja kujifunza na baada ya kupata ujuzi wanakwenda kuanzisha ofisi zao, hivyo vifaa hivi vitatusaidia sana”alisema Mrema.

# BOOST YAJENGA SHULE MPYA 2 NA MADARASA 40



*Umaliziaji wa madarasa ya Mradi wa BOOST kwenye shule ya Msingi Mbuyuni.*

Halmashauri ya Wilaya ya Same imepokea jumla ya shilingi Bil 1.86 kutoka Mradi wa kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji kwa shule za Awali na Msingi (BOOST) ambazo zitatekeleza miradi mbalimbali katika shule 10 za Msingi ikiwemo ujenzi wa shule mpya mbili.

Akizungumzia utekelezaji wa Miradi hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Anastazia Tutuba amesema fedha hizo zilipokelewa mwishoni mwa mwezi Mei, 2023 na tayari utekelezaji wa Miradi upo katika hatua za umaliziaji.

Alizitaja shule zilizonufaika na Mradi wa BOOST Wilayani Same kuwa ni Shule ya Msingi Kisima, ambapo panajengwa shule mpya (446,500,000/-),Shule ya Msingi Mgandu ambapo panajengwa pia shule mpya(348,500,000/-).

Shule nyingine ni Mpirani,Turiani na Kwesasu ambazo kila moja imepatiwa shilingi 131,300,000/-kwaajili ya ujenzi wa madarasa matano kila moja, huku shule ya Msingi

Mbono na Ndolwa ambazo kila moja imepatiwa shilingi 181,300,000/- kwaajili ya ujenzi wa madarasa saba kila shule.

“Shule ya Msingi Kikwete imepokea Shilingi 162,600,000/-kwa ajili ya ujenzi wa madarasa sita na Dimbwi, wamepokea shilingi 81,300,000/- kwaajili ya ujenzi wa madarasa matatu,

huku shule ya Msingi Mbuyuni ikipokea Shilingi 69,100,000/- kwaajili ya ujenzi wa madarasa mawili ya kisasa ya Awali "amesema Tutuba.

Mkurugenzi amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Tanzania, Dkt.Samia Suluhu Hassan, kwa kuipatia Same fedha hizo ambazo zitasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza uhaba wa madarasa katika shule za Msingi Wilayani humo na kusaidia ongezeko la shule kwa kujenga shule mpya.

Mwenyekiti wa Halmashauri, Mhe.Yusto Mapande, pia ameishukuru Serikali kwa kuipatia Wilaya hiyo fedha hizo, ambapo amemtaka Mkurugenzi wa Halmashauri na timu yake kuhakikisha kuwa Miradi hiyo inakamilika kwa wakati na kwa ubora unaostahili.

"Sina mashaka Mkurugenzi wangu, nina imani hii miradi itasimamiwa vema na itakamilika kwa wakati na kwa ubora kama ilivyo kwa miradi mingine iliyotekelezwa katika Wilaya yetu"alisema Mhe.Mapande.

Akizungumzia hatua ya Ujenzi iliyofikia kwa sasa Afisa Elimu Msingi wa Wilaya ya Same, Maclaud Mero, alisema Miradi yote ipo katika hatua ya umaliziaji (finishing) na upakaji wa rangi.

# SAME YAPATA HATI INAYORIDHISHA KWA MIAKA MITATU MFULULIZO



*Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Innocent Magayane, akitoa taarifa kwenye kikao Maalum Cha Baraza la Madiwani.*

Halmashauri ya Wilaya ya Same imepata hati inayoridhisha kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka mitatu mfululizo.

Akizungumza katika Kikao Maalum Cha Baraza la Madiwani Cha kujadili Hoja za Halmashauri hiyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Mweka Hazina wa Halmashauri Bw. Innocent Magayane, alisema Halmashauri hiyo imepata hati inayoridhisha kwa miaka mitatu mfululizo.

"Kwa upande wa hoja tulikuwa na hoja 37 ambapo 13 ni za Miaka ya nyuma na kwa mwaka uliokaguliwa wa 2021/22 kulikuwa na hoja 24 tu"alisema Magayane.

Alisema kuwa hata hivyo hoja 18 zimefanikiwa kufungwa, zikiwemo hoja 5 za miaka ya nyuma ambapo hoja zilizobaki 6 ni za kisera, 1 ipo katika vyombo vya uchunguzi na 12 zipo kwenye mawanda ya Halmashauri na utekelezaji wa maelekezo ya CAG unaendelea ili kuhakikisha hoja zote zinafungwa.


Akizungumza katika Kikao hicho Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Bw.Tixon Nzunda, alimtaka Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri kuhakikisha kuwa anatoa ushauri wa mara kwa mara ili kuepusha Halmashauri kuwa na hoja.

“Mkaguzi wa ndani atoe ushauri kuepuka hoja na pale hoja inapotokea pia ijibiwe kwa wakati ili iweze kufungwa mapema"alisema Bw.Nzunda.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Bi.Anastazia Tutuba, alimshukuru Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Bw.Tixon Nzunda, kwa kuhudhuria kikao hicho ambapo pia alimuahidi kuendelea kufanyia kazi hoja zilizobaki ili ziweze kufungwa.

"Nikushukuru Katibu Tawala kwa kuweza kuhudhuria Kikao hiki, pia nikuahidi kwamba maelekezo yako yote nimeyapokea na kwa sasa hoja zilizopo kwenye mawanda ya Halmashauri ni 12 na tunaendelea kuzifanyia kazi ili kuhakikisha zote zinafungwa"Alisema Tutuba.

# SAME YAENDELEA KUFANYA VIZURI KWENYE KUKUSANYA MAPATO



Halmashauri ya Wilaya ya Same imeendelea kufanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vyake mbalimbali vya mapato, ambapo kwa kipindi cha miaka mitatu mapato yameongezeka kutoka Tsh.Bil 2 hadi kufikia Tsh.Bil 3.1.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Bi.Anastazia Tutuba, amewapongeza Watendaji wa Kata na Timu ya kukusanya mapato ya Halmashauri hiyo

kwa kujiwekea malengo ya kuongeza makusanyo na kuyasimamia kuhakikisha yanatekelezeka.

"Nichukue nafasi hii kuipongeza kwa dhati kabisa Timu yangu ya kukusanya mapato ya Halmashauri na Watendaji wa Kata kwa kazi kubwa wanayofanya ya kuhakikisha tunakuwa na ongezeko la mapato kila mwaka" alisema Tutuba.

Hata hivyo Mkurugenzi huyo amewaagiza Watendaji Kata kuhakikisha kuwa wanaendelea kuwasimamia vilivyo mawakala wanaokusanya mapato katika maeneo yao ili kuendelea kuongeza makusanyo.

Mkurugenzi huyo amesema katika kuboresha ukusanyaji wa mapato Mashine za kukusanyia mapato (POS) tayari zinatumia Mfumo wa TAUSI ambao unarahisisha makusanyo na kupunguza upotevu wa mapato.

# SAME YAPONGEZWA KUSIMAMIA MKATABA WA LISHE KWA MAFANIKIO



*Watoto wakifurahia siku ya lishe katika Kijiji cha Ndungu.*

Mkuu wa Wilaya ya Same,Mhe.Kasilda Mgeni, amempongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Bi.Anastazia Tutuba, kwa kusimamia vema Utekelezaji wa Mkataba wa Afua za Lishe na kufanikiwa kufanya maadhimisho ya siku ya lishe (SALIKI) kwa vijiji vyote 100 vya Wilaya ya Same.

Mkuu huyo wa Wilaya alitoa pongezi hizo wakati wa kikao cha Tathmini ya Utekelezaji wa Mkataba wa Afua za Lishe kwa kipindi cha robo ya nne iliyoisha Juni 30,2023, ambapo alieleza kuridhishwa na Utekelezaji wa Mkataba huo kwani hata idadi ya watoto wanaopata chakula cha mchana mashuleni imeongezeka toka asilimia 70 mwaka jana na kufikia asilimia 86.

Akizungumza katika kikao hicho Mkurugenzi Mtendaji alisema, lengo la Halmashauri ni kuhakikisha kuwa asilimia 100 ya wanafunzi wanapata chakula cha mchana shuleni ili kuhakikisha hilo Halmashauri ipo katika ukamilishaji wa sheria ndogo ya kulazimisha wazazi kuchangia chakula cha watoto mashuleni.

“Kuna wazazi wanakaidi kuchangia chakula kwa ajili ya watoto wao mashuleni na hao tunakamilisha sheria ndogo ya kuwabana ili watoto wote wawe wanakula shule”alisema Bi.Tutuba.

Alisema kupitia mapato ya ndani Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imetoa shilingi milioni 56.82 sawa na aslimia 99.3 ya bajeti iliyotengwa kutekeleza masuala ya Lishe.

Alisema kwa sasa wilaya imejikita zaidi katika kupambana na tatizo la udumavu kwa watoto, ambapo asilimia 20 ya watoto 52,349 walio chini ya miaka mitano waliopo Same wanakabiliwa na udumavu.

“Kwasasa tunafuatilia kwa karibu ukuaji wa watoto na tumenunua mbao za kupimia urefu wa watoto (length board)16, kwa kuanzia na zimesambazwa kwenye vituo vya afya na zahanati,hii itatusaidia kujua kama ukuaji wa umri wa mtoto unaendana na kimo chake ili kukiwa na shida tuweze kuchukua hatua mapema”amesema Mkurugenzi huyo.

Kwa upande wake Afisa Lishe wa Wilaya ya Same Bi.Jackline Kilenga,amesema shughuli nyingine za Utekelezaji wa Mkataba wa Afua za Lishe zinazofanyika Wilayani humo ni pamoja na kuhakikisha kuwa wamama wajawazito wanapata vidonge vya kuongeza damu na utoaji wa matone ya vitamin A na dawa za minyoo kwa watoto.

“Tunaendelea kuhamasisha shule kuwa na bustani za mbogamboga kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi pia tumesambaza mbegu za viazi lishe mashuleni ambapo shule zaidi ya 30 zina bustani za mbogamboga” amesema Bi.Kilenga.

Amesema pamoja na mambo mengine pia Wilaya imeendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa wanawake wajawazito na watoto chini ya miaka mitano kuhudhuria kliniki na elimu ya ulaji na ulishaji bora wa watoto

Afisa Lishe amesema kuwa Wilaya imefanikiwa kupima sampuli 2,809 za chumvi ili kubaini kama zina madini joto ambapo sampuli 2,538 zilibainika kuwa na madini joto ambazo ni sawa na asilimia 90.3.

Wilaya ya Same pia imetenga siku mbili za kufanya mazoezi kwa kila mwezi ili kukabiliana na tatizo la uzito uliozidi.

# HELKOPTA YATUMIKA KURUDISHA TEMBO HIFADHINI




*Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Same wakiwa katika picha ya pamoja mbele ya helkopta iliyotumika katika zoezi hilo mara baada ya kukamilika kwa kazi hiyo.*

Serikali imelazimika kutumia helkopta kutafuta makundi ya Tembo na wanyama wengine waharibifu waliozagaa katika vijiji 25 vya Wilaya ya Same na kuwarejesha katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

Zoezi hilo ni utekelezaji wa agizo la Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe.Mohamed Mchengerwa, alilotoa hivi karibuni alipofanya ziara ya kikazi ya siku moja katika wilaya hiyo ya Same ambapo aliagiza mamlaka ya hifadhi za Taifa TANAPA kupeleka Helkopta

katika Wilaya hiyo kusaidia zoezi la kuondoa makundi ya Tembo yaliyozagaa katika maeneo mbalimbali na kuwarejesha katika hifadhi ya Mkomazi.

Oparesheni hiyo inatekelezwa kwa ushirikiano baina ya taasisi nne zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii,Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Same na wananchi wenyeji ambao wanasaidia kuainisha maeneo walipo Tembo.

Akizungumzia utekelezaji wa Oparesheni hiyo, Mkuu wa hifadhi ya Taifa Mkomazi,Kamishna Msaidizi wa uhifadhi Emmanuel Moirana, amesema kwa siku ya kwanza jumla ya makundi matano ya Tembo yamerejeshwa hifadhini.

Mkakati uliopo ni kuendelea na zoezi ili kuondoa changamoto ya mara kwa mara kuripotiwa makundi ya Tembo kuonekana maeneo ya nje ya hifadhi ambao wanaathiri shughuli za kibinadamu"alisema.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni, amepongeza jitihada hizo za Wizara ya Maliasili na Utalii kwa uharaka wa kutekeleza ahadi ya kuondoa Tembo hao hivyo kuwezesha wananchi kuendelea na shughuli za uzalishaji.

Baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Same walioshiriki katika Oparesheni hiyo wamesema kuna idadi kubwa ya Tembo ambao wametoka kabisa kwenye maeneo ya hifadhi na kufanya makazi ya kudumu kwenye maeneo ya vijiji, hali ambayo imesababisha baadhi yao hasa wakulima mwaka huu kukosa kabisa mazao kwani yameliwa na Tembo.

# CCM YAWATAKA WANANCHI KULINDA MIRADI



*Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro,Comred Jonathan Mabihya, akikagua gati ya maji ya Mabilioni kulia kwake ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro Bw.Tixon Nzunda.*

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Kilimanjaro Comred Jonathan Mabihya, amewataka Wananchi Wilayani Same kuhakikisha wanalinda Miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali Wilayani humo.

Mabihya alitoa wito huo wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Kalemawe alipotembelea kukagua ujenzi wa daraja la mawe Kalemawe lililojengwa kwa gharama ya Shilingi milioni 379.

Katibu huyo ambaye alikuwa ameongozana na Kamati ya Siasa ya Mkoa wamefanya ziara ya siku moja ya kukagua Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025).

“Serikali inatumia fedha nyingi Sana kutekeleza Miradi ya Maendeleo na lengo ni kuondoa kero kwa wananchi, hivyo hakikisheni mnatunza Miradi hii"alisema Mabihya.

Akitoa taarifa ya Ujenzi wa daraja la mawe, Meneja wa TARURA Wilaya ya Same Mhandisi James Mnene, alisema daraja hilo limejengwa kwa Tsh.mil 379 na limekamilika kwa asilimia 100."Daraja hilo lina urefu wa mita 36 na upana wa mita tisa na lina uwezo wa kubeba tani 37 bila wasiwasi pia umri wake wa kutumika ni miaka 100"alisema Mnene.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bi.Anastazia Tutuba, amesema Ujenzi huo unachangia ongezeko la mapato ya Halmashauri, ambapo wafanyabiashara hupata urahisi wa kusafirisha mazao na hivyo kuchangia mapato ya Halmashauri.

Kwa upande wake Mwananchi wa eneo hilo Amina Gadi, aliishukuru Serikali kwa kuwajengea daraja hilo kwani limekua msaada mkubwa kwao.

"Tunaishukuru Sana Serikali kwa kutujengea hili daraja ambalo limekuwa msaada mkubwa kwetu,wanafunzi wanavuka kirahisi kwenda shule na wakulima tunasafirisha mazao kirahisi"alisema Amina.

Katika Ziara hiyo Kamati ya siasa ilitembelea Miradi ujenzi wa daraja la mawe,ujenzi wa eneo korofi barabara ya Hedaru-Vunta-Myamba,ujenzi wa Barabara ya Maore-Mpirani-Ndungu.
Miradi mingine iliyotembelewa ni Mradi wa maji Mabilioni -Hedaru,ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na Ukarabati wa mabweni mawili shule ya Sekondari Sam



*Mkuu wa Kitengo cha Matengenezo TANROADS Kilimanjaro,Bw.Benitho Mdzovela akitoa taarifa ya Ujenzi wa Barabara ya Maore-Mpirani-Ndungu(km5) inayojengwa kwa Kiwango cha lami kwa Katibu wa CCM Mkoa,Comred Jonathan Mabhiya,Barabara hiyo inagharimu shilingi Bil.6.3.*

# MAMLAKA YA MJI MDOGO SAME WAIOMBA TARURA KUONGEZA MTANDAO WA BARABARA



*Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo Same,Mhe. Bakari Singo.*

Mamlaka ya Mji Mdogo Same imewaomba Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini(TARURA ) wilayani humo kuongeza baadhi ya barabara za mamlaka katika mtandao wa Barabara zinazohudumiwa na TARURA ili ziweze kuboreshwa.

Ombi hilo lilitolewa katika Kikao cha Baraza la Mji Mdogo na Diwani wa Kata ya Stesheni,Mhandisi Heriel Mjema, ambapo alisema barabara nyingi wameachiwa Mamlaka ya Mji Mdogo kuzihudumia lakini ni kubwa na zinapaswa kuongezwa kwenye mtandao wa TARURA.

“Zipo barabara zina sifa kabisa ya kuhudumiwa na TARURA lakini tumeachiwa Mamlaka ya Mji Mdogo na zinatushinda kuzihudumia vizuri hivyo tunaomba ziongezwe kwenye mtandao wa TARURA ili zihudumiwe vizuri"alisema Mhe.Mjema.

Aidha wajumbe waliomba kujengewa mitaro kwenye barabara zinazohudumiwa na TARURA, ili kupunguza madhara ya maji wakati wa mvua za masika kwani kuna baadhi ya maeneo yanajaa maji kutokana na kukosekana kwa mitaro mikubwa ya kupokea maji.

Akijibu maombi hayo,Kaimu Meneja wa TARURA Wilaya ya Same Mhandisi James Mnene, aliwataka wajumbe wa Mamlaka ya Mji Mdogo kuorodhesha barabara zote wanazotaka ziongezwe kwenye mtandao wa TARURA.

“Kazi ya TARURA ni kuhakikisha kuwa barabara za mijini na vijijini zinakuwa bora,hivyo kama kuna barabara mnaona zinafaa kuingia kwenye mtandao wa kuhudumiwa na TARURA ziorodhesheni tutazipitia na kuziongeza" alisema Mnene.

Kuhusu uwepo wa mitaro Mhandisi Mnene, alisema katika maeneo yote yaliyojengwa kwa kiwango cha lami yamejengewa mitaro na maeneo ya barabara za changarawe yametengenezewa mteremko ambao huruhusu maji kupita pembeni.

Hata hivyo, Mhandisi Mnene alisema Mji wa Same umekuwa ukipokea maji mengi sana kutoka milimani wakati wa mvua, maji ambayo mitaro iliyopo haiwezi kuhimili hivyo TARURA inatarajia kufanya upembuzi yakini kuona namna ya kujenga mitaro mikubwa itakayoweza kupokea maji yote ya mvua yanayotoka milimani bila kuleta madhara kwa wananchi.

Nae Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo Same, Mhe.Bakari Singo, aliwataka Wenyeviti wa Mitaa kushirikiana na viongozi wao wa Kata ili kuhakikisha Barabara hizo zinaorodheshwa na kukabidhiwa TARURA kwa hatua zaidi.

## SHERIA KUWABANA WATORO NA WASIOCHANGIA CHAKULA MASHULENI



*Mwanasheria wa Halmashauri Bi.Upendo Kivuyo ,akiwasilisha Rasimu ya sheria ya Mahudhurio ya lazima na upatikanaji wa chakula cha Mchana Mashuleni*

Katika kuhakikisha kwamba Mkataba wa Afua za Lishe unatekelezwa kwa ufanisi na utoro unakomeshwa mashuleni, Halmashauri ya Wilaya ya Same ipo katika Mchakato wa kutunga sheria ndogo ya Mahudhurio ya lazima na upatikanaji wa chakula cha mchana mashuleni.

Akiwasilisha Rasimu ya sheria hiyo kwenye Baraza la Madiwani, Mwanasheria wa Halmashauri Bi.Upendo Kivuyo, alisema sheria hiyo inalenga kuondoa utoro na kuhakikisha watoto wanapata chakula mashuleni ili kuboresha afya ya mwili na akili.

"Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kikao chako kijadili na kuridhia Rasimu hii ya sheria ndogo ya Mahudhurio ya Lazima na upatikanaji wa chakula mashuleni" alisema Mwanasheria huyo.

Alisema kwa mujibu wa Rasimu hiyo itakuwa ni kosa kwa mzazi au mlezi kwa kutojali au kukataa kuchangia mchango wa chakula cha mchana kwaajili ya mtoto wake awapo shuleni
.
Sheria hiyo imeweka bayana kuwa, kwa mzazi au mlezi atakayebainika kutomudu kulipa gharama za chakula shuleni basi Halmashauri ya Kijiji italazimika kumlipia mtoto huyo.

Hata hivyo Rasimu hiyo imependekeza faini isiyopungua shilingi laki mbili,kifungo mwaka mmoja jela au vyote kwa pamoja kwa mzazi au mlezi atakayeshindwa kuchangia chakula cha mwanaye shuleni au atakayesababisha utoro kwa mwanaye
.
Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mhe.Yusto Mapande, alisema Rasimu hiyo ya sheria imekuja muda muafaka, kwani uchangiaji wa chakula mashuleni umekuwa wa kusuasua sana.

# KATA ZA KALEMAWE NA NJORO ZAPATA MADIWANI WAPYA



*Msimamizi wa Uchaguzi katika Majimbo ya Same Mashariki na Same Magharibi Bi.Anastazia Tutuba (kulia) akimkabidhi hati ya Udiwani, Diwani wa Kata ya Njoro Bw.Omari Abdallah.*

Kata za Kalemawe na Njoro Wilayani Same, zimepata Madiwani wapya katika Uchaguzi mdogo wa marudio uliofanyika Julai 13 mwaka huu, ambapo katika uchaguzi huo waliokuwa wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wameibuka na Ushindi.

Katika Kata ya Njoro Mgombea wa CCM Comred Omari Abdallah, ameshinda baada ya kupata kura 981 akifuatiwa kwa mbali na mgombea wa NCCR -Mageuzi Bw.Raphael Mrutu aliyepata kura 69.

Akizungumzia Uchaguzi huo, Msimamizi wa Uchaguzi katika Majimbo ya Same Mashariki na Same Magharibi Bi.Anastazia Tutuba, alisema katika Kata hiyo ya Njoro
Mgombea Rashid Msuya wa ADC alipata kura 8 na wa mwisho ni Paulo Mshana wa TLP aliyepata kura 6.

Msimamizi huyo alimtangaza Omar Abdallah wa CCM kuwa Diwani wa Kata ya Njoro.

"Jumla ya wapigakura 2495 walijiandikisha kupiga kura na waliojitokeza kupiga kura walikuwa 1070 ambapo kura halali zilikuwa 1064 na kura 6 zilikataliwa"alifafanua Bi.Tutuba.

Kwenye Kata ya Kalemawe aliyekuwa mgombea wa CCM Comred Jofrey Jofrey, alishinda kwa kura 1489, akifuatiwa na mgombea Helena Juma wa TLP, aliyepata kura 107 ambapo mgombea Musa Philipo wa CUF alipata kura 50.

Bi Tutuba alisema wapiga kura walioandikishwa walikuwa 2506, huku waliopiga kura wakiwa 1648, ambapo kura 2 ziliharibika.

Msimamizi huyo alimtangaza Jofrey Jofrey wa CCM kuwa ndiye Diwani wa Kata ya Kalemawe.
“Niseme tu zoezi zima la Uchaguzi lilikuwa la amani na utulivu na uchaguzi ulikuwa huru na haki,na sasa tumepata Madiwani katika Kata zetu mbili zilizokuwa hazina uwakilishi katika Baraza la Madiwani”alisema Msimamizi huyo.

Uchaguzi huo mdogo wa marudio umefanyika katika Kata hizo kufuatia vifo vya waliokuwa Madiwani wa Kata hizo Marehemu Athumani Mbelwa (Kalemawe) na Marehemu Clement Mchomvu (Njoro) .

## WAUGUZI WASISITIZWA KULINDA SIRI ZA WAGONJWA

Wauguzi Wilayani Same wametakiwa kutimiza majukumu yao kwa kuzingatia weledi wa kazi yao, ikiwa ni pamoja na kutunza siri za Wagonjwa.

Wito huo ulitolewa na Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo Dk.Alex Alexander, wakati akizungumza katika Maadhimisho ya siku ya wauguzi Duniani.

Maadhimisho ya siku ya wauguzi Duniani hufanyika Mei 12, ya kila mwaka ambapo Wauguzi hukutana kwa ajili ya kukumbushana majukumu yao.

Dk.Alexander alisema Wauguzi pamoja na madaktari wana jukumu kubwa la kushughulika na uhai

kuhakikisha kuwa mgonjwa anayepatiwa huduma anaondoka akiwa ameridhika na huduma aliyopatiwa.

"Wauguzi na madaktari tunakutana na mambo mengi wakati wa kutimiza majukumu yetu hivyo tunapaswa kulinda siri za watu tunaowahudumia"alisema.

Daktari huyo alisisitiza Wauguzi pia kuwa waaminifu na waadilifu wakati wakitekeleza majukumu yao ya kuwahudumia wagonjwa.

Akizungumzia historia ya maadhimisho ya siku ya Wauguzi Duniani,Muuguzi Aramica Mangi wa Hospitali ya Wilaya ya Same, alisema siku hiyo huadhimishwa Kama kumbukizi ya siku ya kuzaliwa ya Muuguzi Florence Nightingale, ambaye ndiye muasisi wa fani ya Uuguzi Duniani.

## WANANCHI SAME WASHAURIWA KULIMA PARACHICHI ZINAZOKOMAA MAPEMA

Wananchi Wilayani Same Mkoani Kilimanjaro, wameshauriwa kuacha kilimo cha mazoea na badal yake wawe na mtazamo chanya wa kulima mazao yanayoendana na soko la sasa.

Kauli hiyo inakuja baada ya zao la tangawizi linalolimwa kwa wingi zaidi Wilayani Same kuoneka na kushuka bei na kusababisha hasara kwa wakulima wa zao hilo ambalo gharama yake ya uzalisha ji ni kubwa ukilinganisha na mazao mengine.

Ushauri huo umetolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mhe.Yusto Mapande, wakati akizungumza katika Kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika Mei 5,2023.

Mwenyekiti alishauri wananchi hao kulima zao la parachichi kwani maeneo ambayo tangawizi ilikuwa ikilimwa ni maeneo yanayoweza kurutubisha pia zao la parachichi ambalo kwa sasa linafanya vizuri sokoni.

“Same tunataka tuwe na mazao mawili ya kimkakati ambayo ni parachichi za muda mfupi kwa maeneo ya milimani na zao la mkonge kwa wananchi wa ukanda wa tambarare” amesema Mhe.Mapande.

Akichangia hoja hiyo Diwani wa Kata ya Ruvu, Yaigongo Mrutu , amesema parachichi ni zao leny soko kubwa ndani na nje ya nchi hivyo wamelibeba kama zao la kimkakati kwa hiyo, wataendelea kuhamasisha wananchi kuwekeza kwenye kilimo cha mazao hayo.

Wamesema uwepo wa zao hilo utatatua changamoto kubwa ya anguko la bei kwenye zao la tangawizi, ambalo kwa sasa halina soko na bei yake kuwa chini na wakulima kutumia muda mrefu kulihudumia lakini hawapati faida kwani awali tangawizi ilikuwa inauzwa Tsh.3,000/- kwa kilo lakini kwa sasa limeshuka hadi Tsh.400 kwa kilo.

Kwa Upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Anastazia Tutuba, amesema tayari Kata ya Chome Wilayani humo imeshaanzisha vitalu vya parachichi

zinazokomaa muda mfupi na kushauri wananchi wengine kupata miche kutoka Chome wakati Halmashauri ikihamasisha Kata nyingine kuanzisha vitalu vya miche.

“Kwa upande wa uhamasishaji wa kilimo cha katani tayari tumetenga ekari 3,000 katika Kata ya Makanya na wawekezaji wameshapatikana hivyo tunatarajia eneo lile ndio liwe la mfano kwa kilimo cha Mkonge”Amesema Tutuba.

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA





*Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro Jonathan Mabihya, (pichani kushoto) akiotesha mti katika eneo la Kirinjiko panapojengwa Hospitali mpya ya Wilaya ya Same na picha kulia inamuonyesha Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa 2023 Abdalla Shaib Kaim akipanda mti katika eneo hilohilo wakati Mwenge wa Uhuru ulipokimbizwa Wilayani Same.*



*Muuguzi wa Kliniki ya mama na mtoto katika hospitali ya Wilaya ya Same,akimpima Urefu mtoto ili kujua hali yake ya ukuaji wa umri na kimo.Halmashauri ya Wilaya ya Same imenunua vibao maalum 16 vya kupima urefu wa watoto katika kutekeleza Mkataba wa Afua za lishe ili kuhakikisha ukuaji bora wa watoto.*



*Watoto katika Wilaya ya Same wakiandamana katika kuadhimisha siku ya Mtoto wa Afrika ambayo huadhimishwa Juni 16 ya kila mwaka,katika maadhimisho hayo wazazi wamehimizwa kuhakikisha wanawalinda watoto dhidi ya ukatili.*



*Afisa Mifugo wa Kata ya Stesheni,Asimwe Buhemuka, akijiandaa kutoa chanjo ya ugonjwa wa kimeta (Anthrax kwa Ngamia wanaofugwa katika Kata hiyo.*





*Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro Bw.Tixon Nzund,a akimkabidhi fedha Mkazi wa Kata ya Mwembe Bi.Zuhura Hassan (Maarufu kama Bi.Kitoto) kama ahsante baada ya bibi huyo anayeishi jirani na inapojengwa Ofisi ya Tarafa ya Mwembe –Mbaga kujitambulisha kwamba amekuwa mlinzi muhimu wa vifaa tangu Ujenzi huo uanze.Katibu Tawala alikuwa katika ziara ya kukagua Miradi ya Maendeleo Wilayani Same.*



JARIDA MTANDAO WILAYA YA SAME

LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
S.L.P 138,SAME

Mhariri Mkuu:Anastazia Tutuba

Mhariri wa Habari:Amina Sangawe

Toleo la Juni, 2023 www.samedc.go.tz
email: ded@samedc.go.tz

samedc2022 Same DC